



## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

JUMATANO, 23 NOVEMBA, 2022.

### **TAARIFA YA HALI YA UPUNGUFU WA UMEME NA MIPANGO YA KUKABILIANA NAO.**

TANESCO inapita katika kipindi kigumu cha upungufu wa umeme unaosababishwa na ukame na matengenezo ya mitambo. Jumla ya megawati 300 hadi megawati 350 za umeme zimepungua katika uzalishaji kwa siku za hivi karibuni.

Vituo vya kufua umeme vilivyoathiriwa na ukame ni Kihansi kinachozalisha megawati 17 badala ya megawati 180 kwa hiyo megawati 163 hazizalishwi; Pangani kinachozalisha megawati 10 badala ya megawati 68 kwa hiyo megawati 58 hazizalishwi; Mtera kinachozalisha megawati 75 badala ya megawati 80 kwa hiyo megawati 5 hazizalishwi na Nyumba ya Mungu kinachozalishaji megawati 3 badala ya megawati 8 za umeme, kwa hiyo megawati 5 hazizalishwi.

Vilevile, vituo vilivyo katika matengenezo ni Kidatu kinachozalisha megawati 150 badala ya megawati 200, kwa hiyo megawati 50 hazizalishwi; Ubungo III kinachozalisha megawati 37 badala ya megawati 112, kwa hiyo megawati 75 hazizalishwi na Kinyerezi II kinachozalisha megawati 205 badala ya megawati 237, kwa hiyo megawati 32 hazizalishwi. Kwa hiyo jumla ya umeme ambao hauzalishwi kwa sababu ya ukame na matengenezo ni megawati 388 za umeme hadi kufikia tarehe 23 Novemba 2022.

### **MIPANGO YA MUDA MFUPI**

Kuharakisha matengenezo ya mitambo hii ambapo jumla inatarajia jumla ya megawati 90 zitapatikana kama ifuatavyo;

- Kuharakisha matengenezo ya mtambo mmoja katika kituo cha Ubungo III ili kuingiza megawati 35 za umeme tarehe 25 Novemba 2022;
- Kuharakisha matengenezo ya mitambo miwili ya Ubungo III ili kuingiza megawati 40 za umeme mwishoni mwa Disemba 2022;
- Kukamilisha matengenezo ya mtambo mmoja wa kituo cha Kidatu ili kuingiza megawati 50 za umeme tarehe 30 Novemba 2022;
- Kuharakisha ufungaji wa mitambo miwili katika kituo cha upanuzi cha Kinyerezi I ili kuingiza megawati 90 za umeme kabla ya mwisho wa mwezi Disemba 2022.

Hii ni kama ukarabati ukikamilika kama ulivyopangwa, itatupatia jumla ya megawati 277 kwenye uzalishaji na kupunguza kadhia hii ya umeme.

### **MIPANGO YA MUDA WA KATI**

- Tunategemea mtambo mwingine kuanza kufanya kazi katika kituo cha upanuzi cha Kinyerezi I ili kuingiza megawati 90 za umeme mwezi Februari 2023 na kufikisha jumla ya megawati 337 za umeme.

Tutaendelea kutoa taarifa ya hali ya umeme na ratiba ya upungufu wa umeme kadri inavyozidi kuimarika kupitia mikutano na waandishi wa habari, mikutano ya kwenye mtandao (club house), tovuti yetu ya [www.tanesco.co.tz](http://www.tanesco.co.tz), kwenye magroup ya whatsapp ya wateja, magazeti na ujumbe mfupi wa maneno (SMS).

**IMETOLEWA NA;**

**KURUGENZI YA MAWASILIANO NA UHUSIANO KWA UMMA,  
TANESCO - MAKAO MAKUU.**